**KENYA**

# Kongamano Kuhusu

## *Kuimarisha mazungumzo na wadau katika sekta ya misitu nchini Kenya*

Dhana fupi

---

**A. Utangulizi**

Benki ya Dunia, kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya, inaandaa Kongamano la siku nne kwa mada ya Kuimarisha Mazungumzo na Wadau katika sekta ya misitu nchini Kenya. Kongamano hili litatoa jukwaa kwa ajili ya kutathmini njia bunifu za matatizzo ta muda mrefu kuhusu masuala ya usimamizi wa misitu, matumizi ya ardhi na upatikanaji wa haki, kukuza mbinu za kijamii, kama vile usimamizi shirikishi wa misitu, na kuwezesha ushirikiano kati ya jamii, serikali na serikali za mitaa. Pia, itakuwa kuchangia kuendelea mchakato wa mazungumzo kati ya serikali na wadau mbalimbali katika sekta ya misitu nchini Kenya.

**B. Malengo**

Malengo makuu ya Kongamano hili ni: (i) kuwezesha mjadala wa kubuni ushirikiano wa kudumu kati ya wadau muhimu katika sekta ya misitu nchini Kenya; na (ii) Kuangazia mafunzo ya kitaifa na kimataifa na njia bora zaa usimamizi wa rasilimali za misitu kwa ajili ya ufumbuzi wa mbinu za kupunguza umaskini, kuboresha hali ya maisha na kustawisha mazingira. Inatarajiwa kwamba matokeo ya Kongamano yatachangia ustawi endelevu wa misitu kilingana na muundo wa Mpango wa Taifa ya Misitu (NFP) mchakato ulioanzishwa mwishoni mwa mwaka jana.

**C. Mwanzo**

*a. Mtazamo wa Sekta*

Rasilimali ya mali asili nchini Kenya ni msingi muhimu katika uchumi wa taifa hili. Hata hivyo mali asili hii inakumbana na changamoto ambazo zinaiweka katika hatari ya kuangamizwa na majanga kama vile ukame na mafuriko. Ongezeko la Mahitaji ya ardhi na rasilimali zingine limeongezea shinikizo kwa mali asili nchini haswa misitu na maji.taifa hili bado linakumbwa na uhaba mkubwa wa maji huku usimamizi wa misitu ukiathiri rasilmali ya maji na zaidi hali ya maisha, maendeleo na ustawi .

Usimamizi duni  na kunyakuliwa kwa  kwa misitu  kuimepunguza kiwango cha misitu nchini kutoka asilimia 10 ya ardhi yote ya Kenya ilivyokuwa wakati wa kujinyakulia uhuru mwaka 1963 hadi asilimia 6.9 kwa sasa. Changamoto kuu ya kudumisha na kuimarisha mazingira na uwepo wa  misitu ya Kenya inahusiana na suala gumu la  ardhi na umiliki wake. Kwa vizazi vingi maeneo ya misitu chini yamekuwa chanzo cha mizozo ya umiliki wa  ardhi na ugavi wa rasilmali muhimu kwa jamii husika jinsi ilivyo katika mataifa mengi duniani.Katika  baadhi ya matukio, maeneo ya misitu yamekaliwa na jamii ambazo zimesisitiza kwamba zina haki kutoka kwa mababu zao kuishi na kutumia misitu. Hali hii imepelekeakuwepo kwa  utata wa muda mrefu kati ya  taasisi za serikali na jamii zinazoishi karibu na misitu

Kutambua kuwepo kwa matatizo makubwa   katika sekta ya misitu  kulipelekea Serikali ya Kenya kuandaa Sera ya misitu (Forest Policy )  na Sheria ya Misitu(Forest Act), zilizoidhinishwa na bunge mwaka 2005.  Malengo makuu ya mageuzi katika sekta ya misitu yalikuwa kuongeza ufanisi, kuhakikisha ulinzi na matumizi endelevu ya misitu, na  kupunguza umaskini.  Kwa hivyo, Kuimarisha utawala wa misitu, ni muhimu kwa ajili ya mafanikio ya juhudi hizi. Sheria ya misitu ilitilia maanani  usimamizi shirikishi wa misitu, ambapo vyama vya kijamii vinavyotunza misitu (CFAs) vitatambuliwa kama washirika. Aidha inapendekeza ushirikiano  wa sekta ya kibinafsi  kuongeza ushindani wa sekta ya misitu. Sambamba na hayo , Kenya anashiriki katika mikataba mbalimbali ya kimataifa kama vile mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa (UNFCCC), Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu  ya ukame majangwa (UNCDD) , mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu  Biolojia (UNCBD), na mipango kama vile Forest Carbon Partnership Facility na mpango wa UN-REDD. Ushirikiano wa aina hii unatoa fursa  kwa jamii kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa rasilmali hii muhimu na hivyo kupunguza  uharibifu wa misitu kutokana na ukataji miti.

*b. Mradi wa usimamizi wa mali asili kwa udhamini wa benki ya Dunia (NRMP)*

Mradi wa NRMP uliotekelezwa kati ya  2007 - 2013, ulilenga  kuimarisha sera na shughuli zingine  ili kuhakikisha usambazaji maji wa kudumu , kuboresha kilimo cha unyunyiziaji, na kuboresha usimamizi wa  misitu. Kwa ujumla, ilipata matokeo ya kuridhisha. Zaidi ya  watu 145,000 wa vijijini wamefaidika kwa kuilimo cha unyunyiziaji au kwa njia ya miradi midogo ya -jamii inayoiinua hali ya maisha na kutoa fursa ya mapato zaidi kwa jamii tengwa za kando ya misitu.. Aidha,takriban hekta  320,000  misitu sasa zinasimamiwa  kulingana na mipango iliyoidhinishwa ya usimamizi wa misitu. Mradi huu  pia alithibitisha masomo kadhaa muhimu.

Masomo haya ni pamoja na kwamba usimamizi endelevu wa misitu katika maeneo mengi ya Kenya unakabiliwa na migogoro na / au kutokuwa na uhakika kuhusu haki za wananchi na uhusiano wa serikali ns rasilimali za msitu maeneo yaliyoko karibu.

Mwaka 2013, baadhi ya wenyeji wa jamii za Cherangany na Sengwer wanaoishi katika vilima vya Cherangany waliwasilisha ombi kwa Jopo la Ukaguzi la Benki ya Dunia. Wenyeji hao walidai kwamba walikuwa wameondolewa kwa lazima kutoka ardhi yao ndani ya misitu kutokana na mradi wa NRMP, na kwamba haki zao za kitamaduni hazikutambuliwa wala kulindwa wakati wa kutekelza mradi huo.
Jopo liligundua kuwa uhamisho huo haukuwa na uhusiano na mradi wa NMRP. Hata hivyo, alibainika kuwa ingelikuwa bora kutoka mwanzo endapo ingetiliwa maanani na kupunguza hatari ya uhamisho huo. Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Dunia ilibain8i kwamba japo kusuluhisha swala kama vile la urithi ni vigumu , inaweza kuwajibika kwa kuongoza na kuwa mshiriki katika kuanzisha mazungumzo muhimu kati ya serikali na jamii zinazotegemea misitu . Ni kutokana na haya ambapo usimamizi wa Benki ya Dunia ulijitolea kuandaa kongamano kwa ushirikiano na Serikali ya Kenya ili kutoa jukwaa kukuza mjadala kati ya serikali na wadau katika sekta ya misitu nchini.

*c. Kujihusisha kwa Benki ya Dunia na Jamii zilizotengwa nchini Kenya*

Benki ya Dunia ina historia ya kujihusisha na jamii zinazoishi katika mazingira magumu namaeneo yaliyotengwa nchini Kenya kwa kuzingatia yaliyomo katika sera yake kuhusu Jamii asili OP4.10 Pia inafanya kazi na makundi ya wanyonge na waliotengwa (VMGsvijijini, , kitaifa na kimataifa katika michakato mbalimbali, hivi karibuni na Forest Carbon Partnership Facility (FCPF) na tathmini inayoendelea ya sera za Benki ya Dunia . Kwa mfano ,wawakilishi wa jamii tengwa nchini Kenya walishiriki kikamilifu katika mazungumzo FCPF yaliyoandaliwa mjini Arusha, Tanzania mwezi Aprili, 2012 na mwishoni mwa mwaka 2014. Mazungumzo mengine ya jamii asili yamekuwepo Februari 2015, Cape Town Desemba 2013, Jo'burg Novemba 2014na mashauriano zaidi yamepangiwa kufanyika Yaounde Cameroon baadaye Mwezi huu wa Machi 2015.

**D. Kongamano: Mjadala, Mafunzo na ugawanaji wa maarifa**

*a. Matokeo yanayotarajiwa*

Kutokana na masomo kufuatia mashauriano mbalimbali katika siku za awali, haswa Januari 2015 kwenye Mdahalo wa kitaifa kwa jamii zinazotegemea misitu kama sehemu muhimu ya mpango wa kitaifa wa maendeleo ya misitu, Inatarajiwa kwamba washiriki wataimarisha weledi wao wa maoni tofauti na utata wa usimamizi wa misitu, matumizi ya ardhi, haki na mambo ya urithi, kujifunza kutoka kwa mifano

ya vijijini, kitaifa, na kimataifa; na kutoa mapendekezo thabiti kwa njia iliyo bunifu na inayoimarisha ushirikiano kwa njia inayoleta pamoja wadau katika usimamizi wa rasilmali ya misitu nchini.Kwa hivyo, kongamano hili sio mwisho bali ni mojawapo tu ya mijadala muhimu.

. Aidha, Kongamano litatoa ripoti iliyo na hiyo v mapendekezo yanayoweza kufuatiliwa na kuchochea mazungumzo ambayo tayari yameanza kati ya serikali na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja jamii zinazotegemea misitu kote nchini . Pia litatoa maudhui ya sera muhimu kwa Mpango wa kitaifa wa misitu yanayoweza kutumiwa na serikali katika shughuli zake na jamii zinazotegemea misitu.

*b. Wakati na sehemu ya Maandalizi*

Kongamano litafanyika kwa kipindi cha siku nne, kati ya Machi 03-06, 2015 katika Boma Inn Hotel mjini Eldoret. Kama ilivyokubaliwa, Benki ya Dunia itagharamia mkutano wa ndani ya ukumbi kwa washiriki wapatao 100 wa jamii zinazotegemea misitu kutoka kaunti 14 tarehe 3 Machi 2015. Mkutano huu, utakaotangulia Kongamano halisi, utalenga kujumuisha na kuimarisha zaidi memoranda na maswala ambayo jamii zitawasilishwa kwenye kongamano. Mkutano huo wa siku moja pia utarejelea Mdahalo wa Januari mwaka 2015 na kuchagua watakaozungumza katika ufunguzi wa kongamano.

*c. Maandalizi na mpangilio*

Kikundi kutoka Benki ya dunia kwa kushauriana na Wizara ya Mazingira, Maji na Mali Asili itasaidia katika maandalizi ya kongamano kwa ushirikiano na wadau wengine. (tazama chini).
Kiongozi wa jukumu hili kutoka Benki ya Dunia anajukumiwa kuratibu na kupanga ghafla hii kwa ushirikiano wadau muhimu huku akitoa habari muhimu kwa usimamizi wa Benki kutambua na kuwaalika washiriki ,kukodisha watakaowezesha kongamano, na kuhakikisha kwamba ripoti kamili kuhusu kongamano imetayarishhwa kikamilifu na kuwasilishwa kwa usimamizi wa benki. Vikosi vya Benki ya Dunia nchini Kenya na Washington D.C zitatekeleza shughuli zinazohusiana na maandalizi, mwaliko wa washiriki na kutoa misaada mingine inayohitajika.

Vikao Kongamano vitafanyika kwa Kiingereza na tafsiri kufuatia kwa Kiswahili.
Jopo maalum litateuliwa kutoka makundi mbalimbali ya wadau yatakayoshiriki katika Kongamano na kujukumiwa kuandaa ripoti rasimu ya mapendekezo yanayoweza kutekelezwa, na maamuzi yatakayoafikiwa katika kikao cha siku ya mwisho ya Kongamano. Jopo hili litasaidiwa na wawezeshaji wawili ambao kazi yao ni kuendesha kongamano na kuhakiksha matokeo yanayotarajiwa yameafikiwa. Wawezeshaji hawa watawasilisha ripoti kamiliya matukio ya Kongamano kwa TTL katika muda wa usiozidi majuma mawili baadaye.

*d. Mashauriano na muundo wa Kongamano*

Jamii zinazotegemea misitu, jamii zilizotengwa, '(VMGs') viongozi, Mashirika ya serikali katika ngazi ya kitaifa na county, Tume za Kikatiba, sekta ya kibinafsi, na wadau wengine muhimu wana jukumu muhimu sana katika maandalizi na kufaulu kwa Kongamano . Ili kuhakikisha kwamba maandalizi ya Kongamano yanashirikisha mazungumzo yasiyo rasmi yaliandaliwa Januari na Februari kubuni ajenda ya Kongamano. Wawakilishi kutoka county 14 zajamii zinazotegemea misitu , jamii zilizotengwa na viongozi wa jamii zilizo karibu na misitu walialikwa kushiriki mazungumzo hata.Mazungumzo haya pia yanasaidia kuthibitisha na kuhalalisha orodha ya wazungumzaji katika kongamano ili kuhakikisha usawa na uwazi.

*e. Kushiriki*

Kongamano linatarajiwa kushirikisha wadau katika sekta ya misitu wa ngazi zote nchini Kenya. Wao ni pamoja na: (i) jamii zilizotengwa na jamii zinazotegemea misitu, (ii) vyama vya kijamii vya usimamizi wa misitu na makundi yanayotumia misitu, (iii) Wawakilishi wa serikali wakiwemo wizara ya Mazingira, maji na mali asili, Idata ya misitu nchini, Huduma kwa wanyama pori, Tume huru za kikatiba kama vile Tume ya Ardhi, na zinginezo kutoka county na serikali kuu

(iv) Mashirika ya kijamii ya kitaifa na kimataifa, yakiwemo Amnesty International, Forest People’s Programme, Katiba Institute, IUCN, ACT, SKWT na mengineyo, (v) wawakilishi wa sekta ya kibinafsi, (vi) Washirika wa Maendeleo; na (vii) wataalamu wa kimataifa kutoka Tanzania, Ghana, Indonesia, Mexico na Marekani.

*f. Vigezo kwa ajili ya uteuzi wa wawakilishi wa jamii*

Washiriki wa jamii katika Kongamano watachaguliwa kutoka kaunti mbalimbali ambazo zina jamii zinazotegemea misitu. Inatarajiwa washiriki hao kuwa na ujuzi wa hali ya juu ya masuala ya ya jamii zao na kuonyesha uwezo wa ufasaha kuwasilisha masuala haya katika lugha inayoeleweka vyema kwa jamii hiyo. Washiriki ambao awali wamewahi kufanya kazi na Benki ya Dunia wataalikwa ili kuendeleza mazungumzo katika kongamano.wa. Swala la usawa wa kijinsia na kuwakilishwa kwa vijana kutoka maeneo husika pia litatiliwa maanani. Washiriki wanatarajiwa kuwakilisha maoni ya jamii zao na lazima kuwa na utaratibu pamoja na njia za kitamaduni za kuwasiliana na jamii zao baada ya kongamano. jadi, kuwasiliana nyuma majimbo yao. Washiriki kutoka maeneo ya NRMP watapewa kipaumbele.

Washiriki wnaotarajiwa katika kongamano ni kama ifuatavyo:Jamii zinazotegemea misitu, mashirika ya kijamii ya kitaifa na kimataifa, kampuni za kibinafsi hasa zinazotengeneza mbao, maafisa wa serikali, tume huru za katiba, wataalamu wa kitaifa na kimataifa wakiwemo wasemaji na wajadili,washirika wa maendeleo na wafanyikazi wa benki ya dunia . Inatarajiwa kwamba idadi ya washiriki itafikia takriban watu 250.

*g. Agenda*

Kongamano hili la siku nne litatoa fursa kwa wadau mbalimbali kubadilishana maarifa na masomo juu ya njia bora za: (i) kupata ushirika wa kikamilifu wa jamii hasa zinazotegemea misitu katika usimamizi wa misitu, na (ii) kuangazia na kushughulikia matumizi ya ardhi na haki za ardhi, masuala yanayoathiri usimamizi wa misitu kwa ujumla,sawa na jamii zinazotegemea misitu

Majadiliano haya yana msingi wake kutoka kwa msururu wa warsha na mijadala ambayo tayari imeandaliwa na serikali ya Kenya ya kushirikisha jamii katika usimamizi wa misitu, utawala wa rasilimali ya misitu, na matumizi ya ardhi na masuala ya haki za ardhi. Hasa, ni kufuatia Mdahalo wa kitaifa kwa jamii zinazotegemea misitu ulioandaliwa na Wizara ya Mazingira, Maji na Maliasili (MoEWNR) kuanzia Januari 19-21, mwaka 2015 mjini Nakuru na kushirikisha jamii zinazotegemea misitu kutoka kote nchini Kenya.

Jamii hizo ni pamoja na Ogiek na Sengwer kutoka county kumi za Nakuru, Narok, Kericho, Nandi, Baringo, Uasin Gishu, Elgeiyo-Marakwet, Trans Nzoia, Pokot Magharibi na Bungoma.

Mkazo kuu itakuwa juu ya mazungumzo kuendelea ili kubaini njia bora za kuongeza ushiriki wa jamii zinazotegemea misitu katika usimamizi wake na mbinu za kusuluhisha swala la umiliki wa msitu na upatikanaji wa haki. Kwa hivyo, ajenda Kongamano italenga vikao vya kubadilishana maarifa na masomo miongoni mwa wadau watakaoshiriki ikiwa ni pamoja na jamii, serikali za mitaa na kitaifa , sekta binafsi, washirika wa maendeleo, mashirika ya kijamii / NGOs na wataalamu wa nchini na wa kimataifa. Baadhi ya mada muhimu ya mijadala itakuwa ni pamoja na: (i) Kushirikisha wadau kikamilifu katika usimamizi wa maliasili ya misitu na; (ii) Faida kugawana; (iii) Kupata taratibu madhubuti na zinazofaa kwa ajili ya kutatua tatizo la kihistoria la matumizi na haki za ardhi (iv)Masuala ya taasisi, sera na sheria kuhusiana na sekta ya misitu na (v) Kurejelea yaliyojiri katika Mdahalo wa kitaifa.

*h. Gharama*

Kongamano hili litagharamiwa na Benki ya dunia kwa usaidizi wa kifedha kutoka Jumuiya ya Ulaya.